

UKIUKAJI WA HAKI ZA BINADAMU HAUKUBALIWI KWENYE

Shamba letu linahimiza usawa na heshima miongoni mwa wanachama kwa sababu hii inawapa uwezo wa kuboresha maisha yao na kulinda mazingira wanamoishi na kufanyia kazi.

Ikiwa kikundi – matendo, sheria na sera zetu – zinadhuru mtu yeyote, tunataka kuiweka sawa na kuwasaidia wale walioathirika.

Ifichue, isuluhishe na ikomeshe! ✓



MASUALA YA HAKI ZA BINADAMU NI:

Tabia inayodhuru mtu yeyote, mahali popote, inayotokana na shughuli, sheria au sera za shamba.

Ifichue, isuluhishe na ikomeshe! ✓



Kuwatumikisha watoto

Kazi ya kulazimishwa

Ubaguzi

Vurugu na unyanyasaji kazini

Kuwatumikisha watoto, kazi za kulazimishwa, ubaguzi na vurugu na unyanyasaji kazini hudhuru watu na shamba.

Ifichue, isuluhishe na ikomeshe! ✓

UNAPASWA KUWASILIANA NA NANI?



Kamati ya Malalamiko na Kamati ya Kutathmini-na-Kushughulikia, wakiwemo wanachama wa kikundi au waajiriwa wa shamba, huchunguza ripoti ili kujaribu kurekebisha madhara yoyote na kutoa msaada.

Wajumbe wa Kamati:

- Watajibu ndani ya siku 2
- Wataweka ripoti yako kwa siri
- Watakulinda dhidi ya ulipizaji kisasi
- Watashughulikia malalamiko bila kufichua utambulisho

Wajumbe wa kamati yako ni:

Kamati ya Malalamiko:

Kutathmini-na-Kushughulikia:

Wasiliana na (piga simu/SMS):

MASUALA MENGI YANAWENZA KURIPOTIWA

Kitendo kinachomdhuru mtu yeyote, popote pale, kinachotokana na shughuli, sheria au sera za shamba.

Paa la nyumba yangu linavuja maji na licha ya kuwafahamisha wanaohusika uvujaji huo haujarekebishwa.

Mafunzo yanaandaliwa mbali sana nasi, lakini wasimamizi hawafanyi mipango ya kuandaa mafunzo yoyote katika eneo letu.

Bado sijalipwa kwa muda wa ziada wa kazi ingawa nimemjulisha msimamizi wangu.

Nimeshuhudia wafanyakazi wachanga wakibeba mizigo mizito sana kwa umri wao.



Maji taka kutoka shambani bado yanachafua mto ingawa tumemjulisha usimamizi wa shamba kuhusu hilo.


Kuna wanawake wajawazito wanaofanya kazi kwa kutumia viuatilifu na nimemjulisha msimamizi wangu, lakini hakuna mabadiliko.

Nina hofu kuhusu ninavyotendewa kazini na sijui ninapaswa kuzungumza na nani.

JE, NINI KINGINE UNAWENZA KUFANYA?

Ikiwa kikundi – matendo, sheria na sera zetu – zinadhuru mtu yeyote, tunataka kuiweka sawa na kuwasaidia wale walioathirika.

Wajumbe wa K&K na Kamati za Malalamiko wanashirikiana ili kuzuia madhara.



- Unaweza kusaidia kwa:**
- Kuwachagua na kuwasaidia wanachama wa kamati yako
 - Kujiunga na kamati.



Ifichue, isuluhishe na ikomeshe!